# HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA

SHULE YA SEKONDARI PARAKUYO
S.L.P 65.
KIMAMBA-KILOSA
SIMU: 0718-024893/0762115097

TAREHE……………………….

JINA LA MWANAFUNZI
---------------------------------------------
……………………………………………….
……………………………………………….

YAH: **MUONGOZO WA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI PARAKUYO ILIYOPO WILAYA YA KILOSA MKOA WA MOROGORO MWAKA 2020**

UTANGULIZI

Nafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2020. Shule ya sekondari Parakuyo ipo umbali wa KM 63 kutoka Morogoro mjini, kando ya barabara kuelekea Kilosa mjini, kata ya Parakuyo karibu na stesheni ya mkata. Usafiri ni wa basi kutoka Morogoro mjini, unapatikana kituo cha mabasi MSAMVU na nauli ni kuanzia Tshs 6000/=.

Shule hii ni ya Bweni mchanganyiko wasichana na wavulana. Ipo eneo la kijiji cha PARAKUYO kata ya Kimamba na stesheni ya Mkata_Wilaya ya Kilosa.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 06/01/2020 hivyo unataikwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 06/07/2020 Na mwisho wa kuripoti ni tarehe 13/01/2020 ndani ya siku saba. Wanafunzi wa wanatakiwa kufika shuleni kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:30 jioni.

Mara baada ya kufika shuleni watakutana na Mwalimu wa zamu na kusajiliwa katika Ofisi ya Makamu wa Mkuu wa shule. Mwanafunzi atasajiliwa baada ya kuwa amekamilisha maagizo yaliyotajwa katika fomu hii.

Ili mwanao (mwanafunzi) aweze kupokelewa hapa shuleni yafuatayo ni maagizo/maelezo muhimu ya kuzingatia:

1. Nauli ya kuja hapa shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo itolewe na Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi.
2. Mwanafunzi atakapofika hapa shuleni aonyeshe:
   - Cheti cha Uraia cha kuzaliwa
   - Aonyeshe fomu ya kupima afya iliyojazwa na daktari wa Serikali. Imeambatanishwa nyuma.
   - Vifaa vyote vilivyoorozeshwa katika fomu hii.
3. Mwanafunzi awe na fomu hii ya kujiunga ikiwa imejazwa kikamilifu.
4. **Blangeti 1**

**SARE YA SHULE:**

**(A) WAVULANA:**

1. Mashati mawili 2 meupe ya tetroni mikono mifupi.
2. Viatu pea 2 vya ngozi nyeusi na soksi pea 2 nyeupe zisizo na mistari au pambo lolote.
3. Suruali 2 rangi ya kijani rinda mbili
4. Kila mwanafunzi anunue sweta rangi ya kijivu kujikinga na baridi.
5. T-Shirt rangi ya njano au bluu, bukta au kaptula ya rangi ya bluu pamoja na raba rangi ya bluu/nyeusi kwa ajili ya michezo au kazi za nje.
6. Mkanda mweusi wa ngozi
7. Track suti blue au nyeusi (2) yenye mistari mweupe pembeni
8. Vesti nyeupe (2), tochi na saa ya mkononi.
9. Jezi za michezo nyekundu au njano iwe ni bukta na t-shirt yake

**(B) WASICHANA**

1. Mashati mawili (2) meupe ya Tetroni mikono mifupi; au Hijabu - nusu kanzunyeupe(kwa waislamu wanaohitaji).
2. Viatu pea (2) ngozi nyeusi (visigino vifupi na vya kamba) na soksi jozi 2 nyeupe zisizo na mistari au pambo lolote.
3. Sketi 2 rangi ya kijani rinda boksi
4. Nguo za michezo: T-Shirt rangi ya njano au bluu, sketi rangi ya bluu na raba rangi ya bluu au nyeusi.
5. Awe na sweta moja, rangi ya kijivu kujikinga na baridi.
6. Sketi nyeusi 2
7. Track suit bluu/nyeusi moja
8. Nusu kanzu nyeupe 2 za darasani kwa waislam
9. Majuba mawili (2) meusi ya shamba dress.
10. Vesti nyeupe (2), tochi na saa ya mkononi.
11. Jezi za michezo nyekundu au njano iwe ni bukta na t-shirt yake.

**(C) VIFAA VYA CHAKULA**

Awe na bakuli, sahani, kikombe na kijiko.

**(D) MALAZI.**

Mwanafunzi alete:

- Shuka mbili (2) rangi ya bluu kwa wavulana, rangi ya njano kwa wasichana.
- Pazia rangi ya njano wasichana na la blue wavulana
- Chandarua (futi 4), taulo, mto na foronya zake (2) mbili.
- Godoro **futi mbili na nusu kwa futi sita**
- **Ndala za kuogea**

**MAHITAJI MENGINE.**

1. Daftari kubwa 12 (Counter book) za kuanzia.
2. Mathematical set (mkebe), Rula, kalamu ya wino (bluu/nyeusi), penseli, kifutio na begi dogo la kubebea daftari.
3. Kamusi (Dictionary) ya Kiingereza- Kiswahili
4. Jembe jipya lenye mpini, panga, kwanja/fyekeo na ndoo ndogo mbili za lita 10.
5. Sanduku la chuma la kuhifadhia vifaa na kufuli imara.
6. Alete ufagio
7. Aje na Picha za Paspoti.

**MAELEZO MENGINE MUHIMU.**

1. Vifaa kama Redio, kamera, Tape-recorder au simu ni marufuku mwanafunzi kuwa navyo hapa shuleni.
2. Kila mwanafunzi anapaswa kusoma na kuelewa sheria za shule na kuzifuata wakati wote.

Mwisho nakutakia maandalizi mema na karibuni sana Shule ya Sekondari Parakuyo.

**…………**
**P. J. MRUMA**
**MKUU WA SHULE**
***Simu: +255(0) 762115097, 0718 024893***

**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA.**
**SHULE YA SEKONDARI PARAKUYO**

**KANUNI (SHERIA) ZA SHULE:**

Kanuni za shule kama ilivyo sheria za nchi zinaundwa ili kuhakikisha kuwa taratibu zilizokubaliwa na jumuiya zinafuatwa kikamilifu. Aidha sheria hulinda haki na usalama wa watu binafsi na jumuiya.

**1. KANUNI ZA JUMLA**

(i) Yampasa kila mwanafunzi kuwepo mahali atakiwapo kwa wakati na afanye lile linalompasa kwa usahihi na ukamilifu akijua kuwa kufanya hivyo ni wajibu wake.

(ii) Yampasa kila mwanafunzi kujua, kijiheshimu kuzilinda haki zake na wenzake kwa mujibu na kanuni/ sheria za shule.

**2. VAZI RASMI (SARE YA SHULE)**

Vazi rasmi (sare ya shule) kama ilivyoainishwa kwa wavulana na wasichana itavaliwa wakati wote wa:

- ❖ Masomo darasani na muda wote mwanafunzi anapokuwa shuleni.
- ❖ Mhadhara (Baraza la shule).
- ❖ Kutoka nje ya shule kwa shughuli maalumu za kishule au mwanafunzi anapotoka nje ya shule kwa ruhusa maalumu.

Vitu vingine kama kofia, heleni, bangili, mikanda mipana, rangi za kucha na midomo, nywele za bandia, mikufu ya kila aina, hirizi, rozali, kandambili, viatu vya magurudumu, nguo zilizo **chanika** au **kubana** au **nguo fupi** ni marufuku kuvaliwa hapa shuleni.

**3. MIPAKA YA SHULE**

(i) Wanafunzi hawaruhusiwi kuwa nje ya shule wakati wa masomo bila kibali maalumu kutoka kwa mwalimu wa zamu au mlezi.

(ii) Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kukaa au kupumzika au kufanya lolote katika eneo la majani au barabara.

(iii) Ni marufuku wanafunzi kuonekana maeneo ya nyumba za walimu au wafanyakazi wasio walimu bila kupata kibali kutoka kwa mwalimu wa zamu/ mlezi.

(iv) Mwanafunzi haruhusiwi kuingia katika chumba cha walimu (Staff room) ofisi za shule au maabara bila kibali / ruhusa toka kwa mwalimu au mhudumu wa ofisi husika.

(v) Hairuhusiwi kutupa takataka kwenye bustani za maua au viwanja vya shule. Mashimo na madebe ya kuhifadhia takataka yatumike ipasavyo.

**4. MALI YA UMMA**

Kifaa chochote cha shule ni mali ya umma (serikali). Atakayeharibu, kupoteza au kuiba atalipa fidia. Iwapo wanafunzi wengi watahusika itabidi wote walipe fidia kila mmoja kwa nafasi yake.

Mwanafunzi haruhusiwi kuandika katika vitabu vya shule, kuta, madawati, viti, meza, vitanda au ubao wa kufundishia.

**5. KUTEMBELEA WANAFUNZI**

- ❖ Mzazi/mlezi wa mwanafunzi anaweza kumtembelea mwanafunzi kwa sababu maalumu hapa shuleni siku za Jumatano(kuanzia saa 9:30 alasiri hadi saa 11:30 jioni), Jumamosi na Jumapili na siku za sikukuu (kuanzia saa 6:30 mchana hadi saa 11:30 jioni).
- ❖ Mwanafunzi hataruhusiwa kuonana na mgeni yeyote wakati wa masomo au muda tofauti na ilivyoainishwa.
- ❖ Mzazi/mlezi mara tu baada ya kufika shuleni ataonana na mwalimu wa zamu ambapo atamuhudumia kwa niaba ya mkuu wa shule na kumruhusu kuonana na mwanafunzi. Hairuhusiwi kabisa kumpatia mwanafunzi vitu visivyoruhusiwa shuleni.

6. **MAWASILIANO**

- ❖ Mawasiliano yoyote baina ya mzazi na mwanafunzi kwa njia yoyote yafanyike kupitia kwa **mwalimu wa mawasiliano au mwalimu yeyote aliyeainishwa na uongozi wa shule**. Ni **marufuku** kwa mwanafunzi kuwasiliana na mzazi au mlezi kupitia mtu mwingine tofauti na mwalimu wa shule hii. Ikithibitika kufanya hivyo atamsababishia mwanae kufukuzwa shule.
- ❖ Barua zote zielekezwe kwa mkuu wa shule.

7. **MAHUDHURIO**
- Wanafunzi wanatakiwa kuhudhuria shughuli zote za shule kama ratiba ya shule ilivyoainisha. Uvivu haukubaliki hapa shuleni.
- Ni wajibu kila mwanafunzi atii wito wa kengele na kuhudhuria roll-call zote.
- Baada ya likizo wanafunzi wanatakiwa kufika shuleni tarehe iliyopangwa. Kinyume na hili watarudishwa.
- Utoro shuleni ni **mwiko**. Mwanafunzi asipohudhuria vipindi 21 mfurulizo bila taarifa atasimamishwa masomo. Asipohudhuria miezi 3 mfurulizo bila sababu atakuwa amejifuta shule moja kwa moja.

8. **HESHIMA**
- Mwanafunzi anatakiwa kuwa na heshima na mwenendo mzuri awapo shuleni na nje ya mipaka ya shule.
- Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kuamkia walimu/wazazi/wafanyakazi wasio walimu au mgeni yeyote anayepita karibu naye au wanapoingia darasani.
- Wanafunzi wanatakiwa kutii na kuwaheshimu walimu, wafanyakazi na viongozi. Kinyume na hivyo hatua za kinidhamu zitachulúliwa.
- Wanafunzi wote wasimame na washiriki kuimba wimbo wa taifa mbele ya bendera ya taifa.
- Ni marufuku kutumia lugha za matusi,zisizorasmi **(makabila**) shuleni, nje ya shule na uwanjani wakati wa michezo.
- Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu na kukubali tofauti za kidini, kisiasa na kiutamaduni zilizopo katika jamii. Ni marufuku kusababisha hofu, vurugu na kuvunja kanuni za shule kwa kusingizia imani za kidini, ushirikina, siasa na mira au utamaduni. Hatua kali zitachukuliwa.

9. **AFYA**
- Mwnafunzi yeyote mwenye ugonjwa wowote atoe taarifa **mara moja**kwa mwalimu wa zamu au malezi.
- Wanafunzi wote wanatakiwa kunywa maji yaliyochemshwa na kuifadhiwa kwenye chombo kilichosafishwa.
- Ni marufuku kujisaidia nje ya choo au kutupa taka ovyo.
- Wanafunzi wote watatakiwa wale chakula cha shule tu. Ni marufuku mwanafunzi kula chakula kisichopikwa shuleni. Pia hairuhusiwi kuingiza chakula darasani au bwenini. Ni marufuku mwanafunzi kuingia jikoni kujipikia au kupakua chakula mwenyewe.
- Mazingira ya shule ni lazima yawe safi muda wote. Kila mwanafunzi ana jukumu la kufanya usafi wa mazingira na wa kwake binafsi.
- Mwanafunzi mwenye matatizo ya kudumu ya kiafya atatakiwa kuleta uthibitisho kutoka kwa daktari na kuwasilisha kwa makamu mkuu wa shule. Aidha kila mwanafunzi anatakiwa kujaza fomu ya afya iliyoambatanishwa na maelezo haya kabla ya kuja shule.

10. **MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE.**

Mambo yafuatayo hayatakiwi na adhabu yake ni kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule moja kwa moja:
- Wizi, ulevi, kupiga au kupigana.
- Uvivu, kukwepa kazi, kusema uongo, kukataa adhabu na kutoa lugha chafu (matusi).
- Kufanya ngono, kubaka, kuoa au kuolewa, kubeba/kusababisha mimba, usagaji na ushoga.
- Kuonekana kwenye baa, nyumba za wageni au vilabu vya pombe.
- Uvutaji wa sigara, bangi, na matumizi mengine ya dawa za kulevya.
- Kutovaa sare ya shule panapotakiwa na kukwepa masomo au kutofanya mitihani bila sababu maalumu.
- Kukutwa na siraha bwenini na shuleni mf. Visu, rungu, fimbo n.k.
- Kuwasha moto bwenini mf. Pasi ya mkaa, mshumaa, kibatari, n.k.
- Kutumia madawa ya kubadili rangi ya nywele kucha au ngozi yake.

………..

P. J. MRUMA

(Mkuu wa Shule)

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

THE HEADMASTER ,
PARAKUYO SEC. SCHOOL,
P.O.BOX 65,
KIMAMBA-KILOSA.

PART A:
TO The medical officer
…………………………………………………….
…………………………………………………….
……………………………………………………..
REF: MR/MRS/MISS/MS ………………………………………………………………….
Please examine the above named as his/her physical and mental fitness for admission as form one student.

PART B:
MEDICAL CERTIFICATE
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………
I. (a) Eye sight
………………………………………………………………………………………………………

(b)Hearing………………………………………………………………………………………………
…..
(c) Chest
……………………………………………………………………………………………………..
II. Mental and physical fitness
…………………………………………………………………………………………
III.Pregnancy
………………………………………………………………………………………………………………
…….
IV.Other serious diseases
………………………………………………………………………………………………
DATE: ………………………………………………………………………
DESIGNATION: ……………………………………………………………………………